


# YESU NI NANI?

## UUMBAJI

Miaka elfu nyingi zilizopita Mungu aliziumba mbingu na nchi. Akaumba jua, mwezi, nyota, miti yote, maua na nyasi. Akaumba ndege wa angani, samaki na wanyama. Lakini kilichokuwa kizuri sana katika kazi ya vyiumbe vyote vya Mungu kilikuwa mtu.

Mungu aliumba mtu na alipoona kwamba mtu huyo alikuwa peke yake, pia akamuumba mwana mke kutoka ubafu wa mtu awe rafiki na msaidizi wa mume. Mwanamume alimwita Adamu na mwanamke akaitwa Hawa na mumewe.

Shamba nzuri lililoitwa Edeni lilitayarishwa na Mungu. Kuwa makao ya Adamu na Hawa. Hutjui waliishi muda gani kwa furaha. Lakini twajua ya kwamba walipomtii Mungu na kutotenda dhambi walikuwa na furaha.

## MITI MIWILI YA AJABU

Mungu aliweka miti miwili ya ajabu katika bustani la Edeni. Miti hiyo haikuwa ya Adamu wala Hawa, Lakini ilikuwa ya Mungu mwenyewe. Mti mmoja ulikuwa mti wa uzima, kula mti ule ulimaanisha autaonja mauti. Mwingine ulikuwa wa hekima na kujua mema na mabaya. Kula mti ule ilimaanisha kujua mema na mabaya.



Mungu alimpa Adamu uwezo wa kulinda na kutunza vyote bustani. Walikuwa na uhuru wa kula lakini walikatazwa kula kutoka kwa ule mti wa kujua mema na mabaya. Wakiasi Mungu na kula kutoka mti ule, ingekuwa dhambi kuu na wangekufa.

Mungu hakutaka mtu ajue mabaya kwa hivyo aliwakataza kula kutoka ule mti. Jinsi hatutaki watoto wetu wajue maana dhambi na kushiriki katika mambo mabaya duniani. Mungu hakutaka Adamu na Hawa wapoteze utukufu uzuri wa Mungu.

## MALAIKA

Miaka mingi kabla Mungu kuumba ulimwengu alitengeneza mahali paitwapo mbiguni. Mungu aliumba maeifu ya viumbe vya mbinguni kufanya kazi na kumuabudu. Viumbe hivi tunavijua kama malaika. Kulikuwa mpango maaluum kati ya majeshi haya. Nahodha wasaidizi wa malaika Hawa wakuu wa malaika.

## LUSIFA

Nyakati zile za amani mmoja wa wakuu wa malaika alikuwa anaitwa Lusifa. Alikuwa mwenye majivuno na kuasi. Akachukuwa malaika wengi kwa upande wake na pamoja kuanza kupambabna kuchukuwa kwa nguu kiti cha Mungu. Matokeo ni kuwa Mungu alimwuadhibu Lusifa na Malaika walioasi kwa kuwatupa kutoka mbinguni,. Mungu



akatengeneza mahail pa adhabu. Mahali pa adhabu ni ziwa la moto liitwalo Jehanamu.

Baada ya kushindwa Lusifa, aliye pia shetani alimuchukia Mungu na akaanza kutafuta njia ya kulipiza kisasi kwa kujaribu kuharibu kazi nzuri ya Mungu. Aliingia bustanini kwa njia ya nyoka na ustadi akamdanganya Hawa akala tunda la mti wa kuijua mema na mabaya. Hawa akampa Adamu lile tunda naye pia akala.

## HUKUMA

Mungu aliwaadhibu na kuwafukuza kutoka lile bustani la Edeni. Alifanya hivyo kwa maana alijua wangejaribu kula kutoa mti wa uzima na kisha waishi katika dhambi zao milele. Kwa hivyo Mungu hangeshirki na mtu aliyemuumba kushirika naye.

Laana ya Mungu ilifikia jamii ya kwanza kwa sababu ya dhambi ya kuasi. Tokea hapo jamii yao na watu wa ulimwengu huu na mpaka leo, wanazaliwa na tamaa ya kutenda dhambi. Dhambi hii inaonekana muda mfupi baada ya mtoto kuanza kuongea. Ilikuwa huzuni nyingi Mungu alipowafukuza Adamu na Hawa Kutoka nyumba zao nzuri. Hata hivyo Mungu aliahidi kutuma mwana kuwakomboa kutoka kwa laana.

## AHADI YA TUMAINI

Kwa miaka elfu nyingi a hadi hii ilielezwa na



kuelezwa kutoka baba kwa mwana. Kizazi baada ya kizazi walingojea kurudi kwake mwana atakayechukuwa dhambi na kuwaweka huru kutoka hukumu ya dhambi. Kila mara watu walikata tamaa kungojea, Mungu aliwatuma wajumbe, manabii kuwatia moyo wawe na imani na tumaini na waendelea kungoja.

## AHADI YATIMLZWA

Wakati wa utawala wa warumi duniani zaidi ya miaka elfu moja mia tisa iliyopita Mungu alitimiza ahadi yake. Mwana ahadi aliitwaye Yesu maana yake “Mwokozi.” Mungu alisema mtoto huyu mzaliwa wa Maria bikira ni ahdi na mwokozi aliyengojewa na ulimwengu. Malaika wa Mungu alimtokea Maria na kumtayarisha kwa mtoto. Malaika alimwambia itakuwa kuzaliwa kwa kimiujiza kwa sababu hatakuwa na baba wa dunia. Maria alikuwa bado mwana mwali wakati alichukuwa mimba wala hukushiriki kimwili na mtu. Hakuwa mtoto kawaida kwa maana alikuwa mwana wa Mungu mwenyewe aliyekubali kuchukuwa umbo la mwanadamu na azaliwe kama mtoto.

## HUDUMA YA YESU

Yesu alikaa miaka thelathini na tatu katika ardhi ya Israeli. Alionyesha watu upendo wa Mungu kwa kuwapenda wote. Aliponya wagonjwa, vipofu



walifanywa kuona, vilema wakatembea, viziwi wa alisikia na bubu walinena. Alifukuza roho chafu kuwatoka wale waliokuwa wamepagawa nazo, aliwafufua wale waliokuwa wamekufa, na akafanya miujiza mingine mingi ya ajabu. Watu walimpenda, na wengi wakamwamini na kumufuata, lakini wakuu wa dim walifuwa na wivu kwa uwezo wake kuu kwa wata, na wakamvizia kumuua.

## YESU ALSULUBISHWA

Skiu moja walimushika masaa ya asubuhi, wakamuleta mbele za makuhani na viogozi wa siasa, na baada ya kesi na ushahidi usio wa kweli dhidi yake, walimhukumu kifo kwa kumusulubisha, ambayo ilikuwa ni njia ya kirumi ya kuwadhibu wahalifu wabaya.

## YESU ALIFUFULIWA

Walifurahia kwa ushindi wao mkuu, lakini si kwa muda mrefu. Kwa kuwa, baada ya siku tatu baada ya kifo chafe, Yesu Kristo, Mwokozi wa ulimwengu, alifufuka kutoka kwa wafu. Akatoka ndani ya kaburi, na kutokea kwa siku arobaini mbele ya marafiki na wanafunzi wake ambao baadaye walitoa habari za kufufuka kwake kutoka kwa wafu. Yesu baada ya hayo alichukuliwa juu mbiguni ambapo yuko hata leo.

## SABABU YA KUFA KWAKE

Kwanini alikufa? Ilikuwa sababu hakuwa na nguvu ya



kujiokoa? La! Angeliwaita Malaika kutoka mbinguni ili wamuweke huru. Alikuwa mwana mkuu wa Mungu. Lakini alikufa kwa kusudi. Alikufa kwa kuumia kwa adhabu ya dhambi zetu. Alihukumiwa na Mungu, Baba yake mwenyewe, na hukumu ambao tungelihukumiwa nao sisi. Alirudisha ushirika kati yetu na Mungu ambao dhambi ilivunja.

Hii siyo hekaya. Inaweza kusikika kuwa geni kwako, kama hukuisikia mbeleni; Lakini kwetu sisi tulioiamini imekuwa kwetu faraja, furaha na amani. Ikiwa utaamini kuwa Yesu ni mwana wa Mungu, na ya kuwa alikufa kwa ajili yako, nawe pia utapokea musamaha wa dhambi zako, na kupata uzima wa milele. Yesu atakuwa mwokozi wako. Anakupenda. Alikufa kwa ajili yako. Anataka wewe umpende, na umuishie na kuwambia wengine habari hii ambayo nimekwisha kukwambia.

Kama utakataa, na kugeuka utoke kwa upendo wa Mungu utahukumiwa. Hukumu yako itakuwa nini? Utahukumiwa katika ziwa la moto ambalo lilitayarishiwa shetani na malaika wake. Lakini ukiamini utaokolewa kutoka moto huu wa ajabu utakapo kufa. “Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa mwanawe wa peke ili kila mtu amwaminie asipotee bali awe na uzima wa milele.” Yohana 3:16.



## KUPOKEA UZIMA KATIKA YESU

Ikiwa, baada ya kusoma hadithi hii fupi ya uzima wa Yesu na kifo chake, na ukiwa unataka pia kuwa mfuasi wake na kuwa mmoja wa jamii kuu ya Mungu, inamisha kichwa chako sasa na uombe ombi hili fupi:

“Baba uliye mbinguni, naja kwako sasa. Ninakiri ya kwamba mimi ni mwenye dhambi. Ninajawa kuwa nimetenda mambo mengi maovu na dhambi. Siwezi kujibadilisha mwenyewe, lakini wewe unaweza kunibadilisha. Nakuomba unisaidie. Asante Yesu, kwa kufa kwa dhambi zangu. Asante kwa kunichukulia hukumu zangu. Tafadhali unisamehe sasa. Tafadhali uniondolea dhambi zangu. Unifanye mtoto wa Mungu. Nina Kukubali sasa kama mwokozi wangu. Nitakupenda maishani mwangu mwote, nitakuishia, na ikiwa ni lazima nitakufa na wewe. Badilisha maisha yangu, na unifanye mweupe na mtaktifu kama wewe. Katika jina la Yesu naomba, Amina”

Gwen Shaw, End-Time Handmaidens and Servants International